

## **TAARIFA YA SEKTA YA NYUKI KATIKA KAMATI YA USHAURI YA WILAYA (DCC) TAREHE 20/12/2016**

Wilaya ya Chunya ni mojawapo ya Wilaya zinayozalisha asali na nta kwa wingi Tanzania. Uoto wa asili wa miti aina ya miombo ambayo ni malisho ya nyuki na hali ya hewa inachangia sana katika shughuli za uzalishaji. Uwepo wa aina mbalimbali za miti ya miombo inayochanua kwa misimu tofauti husaidia upatikanaji wa chakula cha nyuki kwa mwaka mzima. Shughuli za ufugaji nyuki Wilayani Chunya zinafanyika sana katika tarafa ya Kipembawe japokuwa katika tarafa ya Kiwanja pia yapo maeneo mengi yanayofaa kwa ufugaji nyuki. Uzalishaji wa asali na nta unategemea matumizi bora ya rasilimali misitu, chakula cha nyuki, vifaa bora vya ufugaji, mtaji wa kuendesha shughuli za ufugaji nyuki wenze tija, pamoja na soko la uhakika la mazao ya nyuki.

### **SHUGHULI ZINAZOFANYWA NA SEKTA YA NYUKI**

Sekta ya nyuki inajishughulisha na kutoa elimu na ushauri juu ya ufugaji bora wa kisasa unaoendana na uhifadhi misitu, kukusanya takwimu za ufugaji nyuki, uwezeshaji wa upatikanaji wa mizinga na vifaa vya kisasa vya ufugaji nyuki kiurahisi, kuelimisha na kuwezesha upatikanaji na Matumizi ya vifaa bora vya ufugaji nyuki, Kuwezesha utafutaji wa masoko ya mazao ya nyuki kwa kushiriki na kuwezesha wafugaji nyuki kushiriki maonesho na makongamano mbalimbali ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa masoko na kujifunza mbinu mpya. Tunashirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo kama vile VODA COM Tanzania, makampunin ya uwindaji wa kitalii Wilayani Chunya taasisi za elimu kama vile VETA, taasisi za kidini kama vile Kanisa la Moroviani na mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile African Honey Solution ltd katika kuhakikisha tunainua sekta ya Nyuki Wilayani Chunya ilikuinua kipato cha wananchi kupitia ufugaji nyuki wenze tija.

Taasisis ya African Honey Solution imekuwa mkombozi mkubwa kwa wafugaji nyuki Wilayani Chunya kwani hutoa mikopo ya zana za ufugaji nyuki kwa wafugaji nyuki.

	<b>VIKUNDI HAI VYA UFUGAJI NYUKI WILAYANI CHUNYA</b>				
1	MKOMBOZI	MWAOGA	N	N	H
2	MAKWITA	MAKONGOLOSI	N	N	H
3	WAVIU	MAKONGOLOSI	N	N	H
4	STAMIKO BEEKEEPERS	MAKONGOLOSI	N	N	H
5	MAPOGORO PFM	MAPOGORO	H	H	H
6	FURAHA BEEKEEPERS	SANGAMBI	N	N	H
7	UPENDO MUUNGANO	UPENDO	H	H	H
8	UPENDO BEEKEEPING	UPENDO	H	H	H
9	MANZUKI	UPENDO	N	N	H

10	JITEGEMEE	MAMBA	H	H	H
11	MAENDELEO	MAMBA	H	H	H
12	TUWEZESHANE	LUPA	H	H	H
13	JIKOMBOE	LUPA	N	N	H
14	THJ	NKUNGUNGU	N	H	H
15	ISUNGU	MTANILA	N	N	N
16	LUALAJE PFM	LUALAJE	H	H	H
17	MATWIGA PFM	MATWIGA	H	H	H
18	ARDHIOEVU	MAFYEKO	H	H	H
19	PINDA BEEKEEPERS	BITIMANYANGA	N	H	H

H=HAMNA

N= NDIO

#### IDADI YA MIZINGA

S/N	KIKUNDI/TAASISI/MTU BINAFSI	MIZINGA YA KISASA	MIZINGA YA KIENYEJI
1	VIKUNDI	511	39872
2	KIPEMBAWE BEE RESERVE (TFS)	432	0
3	MR LUKOLOBA	35	0
4	JUMANNE ULEDI	200	1200
5	MR NOAH MCHAFU	60	0
6	SHABANI	50	0
7	AMINI AZIZI	5	0
9	DR MASETA	5	
10	MR BOMBA	10	0
11	MR KAGANGE	40	0
12	AFRICAN HONEY SOLUTION	149	0
13	MH. BOSCO MWANGINDE	5	0
14	MH. REHEMA MADUSA	50	0
15	DANI KADUNDA	10	0

JUMLA	1512	41077
-------	------	-------

MWAKA	ASALI (TANI)	THAMANI (TSHS)	NTA (TANI)	THAMANI (TSHS)
2014/2015	Tani 408.54	2,042,700,000/=	Tani 20.2	101,000,000/=
MAKISIO 2015/2016	Tani 450.2	2,251,000,000/=	25.02	125,100,000/=

### **MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA UFUGAJI NYUKI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO**

Yapo mafanikio kadhaa ambao Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuititia kitengo cha ufugaji nyuki kimeyapata kwa miaka mitano iliyopita ikiwemo kitengo kujitegemea kama sekta kamili, kuongezeka kwa Matumizi ya vifaa bora na vya kisasa vya ufugaji nyuki ikiwemo mizinga ya kisasa, Kuongezeka kwa ushiriki wa wadau mbalimbali katika kuwezesha na kufadhili shughuli za ufugaji nyuki, Kuongezeka kwa wafugaji nyuki na vikundi vya ufugaji nyuki pamoja na Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya nyuki.

Vilevile tumeweza kupeleka sampuli za asali katika maabara zilizokubaliwa kimataifa (accredited laboratory) kila mwaka na majibu kuonyesha kuwa asali yetu haina madhara na inafaa kwa Matumizi ya binadamu.

Kuanzishwa kwa kituo cha mafunzo ya nyuki Kipembawe na hifadhi ya nyuki kipembawe ambapo hadi sasa mizinga 430 imeshatundikwa na kituo hiki kitakachotumika kama eneo la kukusanya mazao ya nyuki na mafunzo ya vitendo.

Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kuititia Kitengo cha Nyuki inatekeleza mradi wa ufugaji nyuki katika vijiji vya Mapogoro, Mamba na Nkung'ungu unaofadhiliwa na Mfuko wa Misitu Tanzania (Tanzania Forest Fund). Mradi huu utasaidia kuwawezesha wafugaji nyuki katika maeneo haya kupata mizinga ya kisasa na vifaa vya kisasa vya ufugaji nyuki.

### **CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SEKTA YA UFUGAJI NYUKI**

- Uvamizi mkubwa wa misitu ya asili hivyo kuathiri shughuli za ufugaji nyuki
- Kuwepo misitu michache iliyotengwa rasmi kwa shughuli za ufugaji nyuki

- Kuendelea kwa Matumizi ya Mizinga ya kiasili yenyе tija ndogo na ambayo si rafiki kwa mazingira na uzalishaji wake ni duni,
- Matumizi ya Vifungashio duni vya asali na mazao mengine ya nyuki, hivyo kuathiri ubora wa asali na nta.
- Uhaba wa wafanyabishara maalum wa mazao ya Nyuki katika Wilaya
- Kutokuwepo maeneo maalum ya kuchakata,kufungashia na kuuzia asali na mazao mengine ya nyuki (collection centers).Tatizo ambalo hupelekeea kuathiri soko la asali kwani ni gharama kwa mnunuzi kukusanya asali kwa mfugaji mmoja mmoja na huwa na mashaka juu ya ubora wa bidhaa.
- Kutokuwepo ushirika wa wafugaji nyuki katika Wilaya ya Chunya, hivyo kupelekeea ugumu kwa wafugaji nyuki kupata mikopo kwa taasisi za kifedha.
- Kutokuwepo kwa taasisi au makampuni yanayoweza kutoa mikopo maalumu ya vifaa vya ufugaji hivyo kukwamisha juhudzi za wafugaji wengi kufuga nyuki kibiashara.
- Bado bidhaa za mazao ya nyuki kutoka Chunya hazijatangazwa vya kutosha japo zinakubalika sana ndani na nje ya mkoa hivyo kuzorotesha upatikanaji wa soko nje ya mkoa.
- Upungufu wa rasilimali fedha, gari la kitengo na upungufu wa wataalamu katika sekta ya ufugaji nyuki.

### **MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

- Tumeendesha warsha ya wadau wa ufugaji nyuki kutoka ndani na nje ya Wilaya ya Chunya na Mkoa wa Mbeya kwa kushirikisha wataalamu mbalimbali
- Kuanzisha manzuki ya Halmashauri itakayotumika kama shamba darasa kwa ajili ya kutolea mafunzo ya ufugaji nyuki wa kibiashara.Lengo nikuwa na angalau mizinga 100 ya kibiashara.
- Kuanzisha maeneo maalum ya kukusanya na kuuzia asali ili kuvutia wanunuzi na kuhakiki ubora wa asali, kwa Kuanzia tumepanga maeneo matatu, ngwala, Mafyeko na Makongolosi.
- Kuhimiza wafugaji nyuki kuunda vikundi na kuvisajili ili wawze kukopesheka na kutambulika rasmi na hatimaye kuunda ushirika wa wafugaji nyuki Chunya.
- Kushauri vijiji kutenga maeneo ya hifadhi ya ufugaji nyuki ilikupunguza kupunguza utegemezi wa misitu, kuhifadhi misitu kwa kuongeza kipato kwa wananchi.
- Kutumia hifadhi ya nyuki Kipembawe kama kituo cha mafunzo kwa vitendo kwa wananchi na eneo la kukusanya mazao ya nyuki.

Asante sana.

**Lucas Theodory  
Kaimu Afisa Nyuki (W)  
Chunya**